TANGAZO LA SERIKALI Na. 46 la tarehe. 24/1/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
(SURA YA 288)

**SHERIA NDOGO**

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA USAFI WA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA MJI WA HANDENI YA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 363 la 2019

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Mji wa Handeni ya Mwaka 2025, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Mji wa Handeni ya Mwaka, 2019 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya aya ya 4

**2**. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika aya ya 4 kwa kuongeza aya ndogo ifuatayo baada ya aya ndogo ya (4):

"(5) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukasimisha jukumu la usimamizi na usafi wa mazingira kwa serikali za mitaa ndani ya Halmashauri na baada ya kukasimiwa mamlaka hayo serikali za mitaa zitaweka utaratibu unaofaa wa kukusanya ushuru wa uzoaji taka na kukusanya taka ngumu kwa ajili ya kuzipeleka dampo.".

Marekebisho ya aya ya 5

**3**. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika aya ya 5 kwa kuongeza aya ndogo zifuatazo baada ya aya ya (4):

"(5) Mtu yeyote ambaye anahitaji kuteketeza vifaa chakavu au bidhaa zilizokwisha muda wa matumizi atalipa gharama ya shilingi laki tatu kwa ajili ya kutumia eneo la Halmashauri.

(6) Mtu yeyote ambaye anahitaji kumwaga maji taka katika eneo maalumu lililotengwa na

Halmashauri atatakiwa kulipa gharama ya shilingi elfu thelathini kwa tripu moja.”.

Marekebisho ya Jedwali

**4**. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza katika sehemu ya kwanza-

(a) katika aya 4, kwa kufuta tarakimu “15.000” na badala yake kuweka tarakimu “10,000”;

(b) katika aya 7, kwa kufuta maneno “nyumba ya kuishi” na badala yake kuweka neno “kaya”;

(c) kwa kuongeza baada ya aya ya 11 aya zifuatazo:

| NA. | ANAYEHUSIKA | KIWANGO CHA ADA |
|---|---|---|
| 12 | Uteketezaji wa vifaa na bidhaa zilizoisha muda wa matumizi | 300,000 |
| 13 | Kumwaga maji taka | 30,000 |

Nembo ya Halmashauri ya Mji Handeni imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia azimio lililopitishwa katika mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji uliofanyika tarehe 7/2/2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

MARYAM A. UKWAJU,
*Mkurugenzi wa Halmashauri,*
*Halmashauri ya Mji*
*Handeni*

MUSSA A. MKOMBATI,
*Mwenyekiti wa Halmashauri,*
*Halmashauri ya Mji,*
*Handeni*

**L.S**

**NAKUBALI**,

Dodoma,
9 Disemba, 2023

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi*